**WIKI YA VIJANA AZANIA FRONT TAREHE 08-14/08/2016**

Kama ilivyokawaida kwenye utaratibu wa Kanisa kuwa na siku maalum ya wakinamama, maombi ya dunia, matengenezo ya kanisa nk, tarehe 08-14 Agosti 2016 Ilikuwa ni wiki ya vijana katika Usharika wetu Azania Front.

Vijana hujumuika pamoja na kushirikiana katika shughuli mbalimbali ambazo huratibiwa na uongozi wa Vijana Usharikani, ambao Mwenyekiti wake ni Eng. Wilfred Moshi.

Uongozi uliandaa Semina ya kiroho kwa ajili ya vijana, mwalimu wa semina hiyo alikuwa Dr. Emmanuel Msechu wa KKKT Msewe. Alifundisha kuhusu Mfumo wa maisha yaliyo katika ulimwengu wa Roho, Imani pamoja na Jinsi tutumiavyo mitazamo yetu katika maisha mf: 'Mtazamo wako unaweza kukufanya ufanikiwe ama usifanikiwe, unaweza ukufanye ukasirike ama uwe na Amani'. Katika Semina hii pia yalikuwepo maombi kwa waliokuwa na shida mbali mbali.

Vijana ndio waliohudumu katika Ibada zote siku ya Jumapili tarehe 14/08 ambayo pia ndio iliyokuwa Kilele cha wiki ya vijana. Vijana walifanya shughuli mbalimbali ikiwemo kuongoza Litrujia, kuwa wazee wa kanisa, maigizo, kuimba kwaya ya Umoja wa vijana iliyo kuwa na mjumuiko wa vijana kutoka katika vikundi tofauti hapa usharikani, n.k

Baadae lilifanyika tamasha la kusifu na kuabudu lililokuwa na Vikundi kutoka ndani na nje ya Usharika, kama Voice Of Angels, Kwaya ya Umoja wa Vijana Azania Front, kikundi cha kusifu na kuabudu Azania front, Kwaya ya vijana Segerea, Vijana Msimbazi, Azania Brothers kutoka Shule ya Sekondari ya Azania pamoja na kikundi cha Edga & Ipiana na baadae kuhitimisha kwa semina na maombezi.